
# Uzuri Wangu



NA MARYCIANA ALEX

2026

# UZURI WANGU

MWANDISHI: MARYCIANA ALEX MAKAMBA

## SEHEMU YA 1

Enjolata alikuwa ni msichana aliyekuwa hataki kuona mtu yoyote kutokana na uzuri wake. wakiwa wamejipodoa isipokuwa kaka yake, chakushangaza hata Boyfriend wake hakuwahi kuona uzuri

wake akiwa amejipodoa kwanini na nisababu gani iliyomfanya afiche uzuri wake?

Siku moja alienda kwenye mahafali ya kaka yake aliyekuwa akihitimu Chuo Kikuu. Alikuwa na mtindo wake akijipodoa hivyo alikuwa akijifunika mtandio mwepesi.

unaweza kumuonyesha njia baada ya kufika kwenye sherehe watu walikuwa wakimshangaa nakusema "mbona huyu dada anaficha uso wake!" siku zote ndiyo alikuwa hivyo.

Ili mlazimu mlinzi kumuita akimuhisi labda atakuwa ni jambazi.

"Lakini ukiona sura unasiku tatu za kuishi namaanisha uta kufa" alisema Enjolata kisha kisha mlinzi anamwambia. "Acha kuwa hivyo nitakuitia polisi nakusema wewe ni muuwaji'' alisema mlinzi.

Enjolata akaamuwa kumuonyesha uzuri wake mlinzi akaingiwa na butwaa. "Kumbe mzuri hivi!" alisema yule mlinzi,

Mlinzi alitokea kumpenda gafla machozi yalimtoka binti Enjolata yakiashiria kifo. "Wewe mshamba unalia kuambiwa unapendwa!" alisema mlinzi huku akimshangaa.

Akiwa anazungumza na mlinzi gafla ujumbe wa maandishi ukaingia kwenye simu yake. "Enjolata toka eneo hili nitakukuta nyuma ya maabara usitoke mpaka nitakapo kuja" ulikuwa ujumbe uliyotoka kwa kaka yake.

Enjolata alitoka nakwenda sehemu ambako alielekezwa na kaka yake. Baada ya sherehe kaka yake Enjolata alimfuata sehemu ile alipo muelekeza ili wapate nafasi ya kupiga picha.

Alimkuta bado Enjolata akiwa anatokwa na machozi huku leso

yake pia ikiwa imelowa kwa machozi aliyokuwa akijifuta.

“kwanini unalia mdogo wangu imekuwaje?” aliuliza kaka yake.

Enjolata ikabidi amuelezee ukweli kuhusu tukio lote zima lililotokea Kaka yake akawa makini kumsikiliza kisha akamwambia.

“Kumbe yeye ndiyo ametaka anasiku tatu za uhai wake tupige picha” aliseema Kaka yake. Baada ya kupiga picha kaka yake alimtakia Enjolata safari njema nakumfunika na mtandiyo vizuri.

**

Enjolata anaamuwa kumtumia ujumbe Boyfriend wake “baada ya siku tatu sitakuwepo kwahiyo usinitafute” lengo ilikuwa nikutimiza kazi iliyokuwa mbele yake machozi hayakuacha kutoka yaliendelea kububujika.

Baada ya siku ya nne kupita machozi yaliachakutoka kwasababu kazi ilikamilika. “Yaani kuna mdada amejiposti ni mzuri kinoma ningekuwa sina girlfriend ninge pambana tu ili nimpate”

“Samahani lakini naomba nione picha ya huyo mdada” alisema Enjolata baada yakuona ile picha anashituka nakukuta niyeye! “inawezekana kaka kaiposti mtandaoni’’ alisama Enjolata huku akiwa anawaza moyoni.

“Je akigundua kama ni mimi itakuwaje namimi sitaki iwe hivyo maana nitampoteza boyfriend wangu”

“wewe mbona kama upo mbali kimawazo alafu, anajina kama lako nayeye anaitwa enjolata ila kidogo anaendana nawewe”

“Acha bhana kuongelea mambo hayo ya picha”

“Hutaki check alivyo na comment za kutosha kila mtu anamuomba namba”

“unatamani ukutane naye anakwa ana?” aliuliza Enjolata.

“ndiyo natamani” alisema mwanaume huyo,

“utapoteza ndoto ya kuniowa” alisema Enjolata kwa utaratibu.

“kwanini unasema hivyo au ndiyo hasira za wivu hizo”

“Hapana sio wivu namaanisha siku ukikutana naye huyo enjolata anakwa ana hakika utakufa nami sitaki iwe hivyo” aliongea Enjolata akiwa na huzuni na kile alichokuwa akikuzungumza.

“umeanza stoy zako za enzi zile za udogo wako ulizokuwa ukisimuliwa na bibi yako” alisema mwanaume boyfriend wake.

**

Ilikuwa takribani miezi miwili ikiwa siku ya ndoa ya dada yake Boyfriend wake na Enjolata. Enjolata aliweka nadhiri akilini mwake “nilazima nipendeze kuliko hata dada yake” Enjolata akiwa chumbani akivaa alipotaka kujipodoa nafsi yake iligoma kufanya hivyo.

“Hapana hawezi kukubali nijifunike mtandio muda wote kwasababu atahitaji sifa kwa rafiki zake” alipokwisha kuwaza hivyo Enjolata aliamuwa kutoka nakwenda kwenye sherehe.

Baada ya kufika

“Enjolata uzuri wako uko wapi mbona unataka kuniaibisha?”

alisema boyfriend wake na Enjolata.  ‶Hebu ngoja nimuite dada hapa akakufanyie make up” aliendelea kuongea  boyfriend wake kisha akaondoka kwenda kumuita dada wa make up.

Punde akaja yule dada ili kwenda kumfanyia make up,

Enjolata alitetemeka moyoni mwake huku akiwa anawasiwasi. ‶Eh mama uliye mavumbini niepushie hili Darrick asione uzuri wangu” Enjolata akavuta pumzi kisha akajisemea mwenyewe silini ‶Atakufa!” alifikilia hivyo kisha anaamuwa kumuambia.

‶Samahani Darrick siwezi kufanya hivyo unavyotaka”

‶kumbe huwezi basi sawa” alisema hivyo kisha akaondoka Darrick. Enjolata akaumia moyo hakutaka kumsikiliza kwasababu hakutaka kupoteza uhai wake, Enjolata akaondoka kwenda nyumbani kwao nakwenye sherehe hakutaka kwenda tena.

**

Tangu kuachana siku hiyo ya sherehe Enjolata hakuwahi kuonana na Derrick na kila mtu akiwa na maisha yake. Ni siku ambayo Enjolata alikuwa amejipodoa kama ilivyokuwa kawaida yake akiwa mjini anatembea, huku akiwa amefunga mtandiyo wake mala anakutana na Derick! na mtandiyo ukadondoka.

Derrick akamtazama Enjolata mkononi Enjolata akawa ameinamisha kichwa ili kuzuiya Derrick asiweze kuona uzuri wake. ‶Unatembeaje unafunga mtandiyo kichwa chako kina akili kweli?” alisema Derrick.

Enjolata akawa akiwaza moyoni ‶naomba asini gundue iliondoke nichukue mtandiyo” aliwaza Enjolata ‶hebu ngoja wewe ni enjolata?” moyo ukimshituka Enjolata kisha akamjibu ‶hapana

umenifananisha” alisema Enjolata.

“lini mpenzi wako ukamsahau au ndiyo dharau ambazo zinafanya usinitazame” alisema Derrick. “unanini usoni mwako?” aliuliza Derrick. “naomba bhana mtandio sitaki mazunumzo nawewe”

“siamini na wala sijawahi kuona mpenzi wako hataki kukuangalia machozi hata kama mmekosana” aliongea Derrick kwa mshangao kisha anampa mtandio wake.

“Huu hapa mtandio wako safari njema” hapo Enjolata akashusha pumzi nakushukuru. Lakini gafla Derrick akarudi nakumshika kwanguvu moja kwa moja kifuani kwake.

Mtafaruku ukaanza huku Enjolata akiwa ameuweka uso wake kifuani kwake Derrick akiwa hataki kuonwa uso wake. Derrick akawa anashangaa! “enjolata uso wako una nini hutaki kunitazama” Derrick aliendelea kuongea.

“Nilisha kusemesha kama ilikuwa nihasira samahani”

“dah! hapa nimebananishwa nitafanyaje” aliwaza Enjolata.

Akaamuwa kuinuwa uso wake na kumtazama Derrick. Enjolata akaona heri afe “waoo kumbe enjolata ni mzuri hivi!” alimbambatisha. Mala baada ya hapo Enjolata akaona ataonwa na wengi akatoka mbio mpaka kwenye kaburi la mama yake.

Enjolata alipofika kwenye kaburi la mama yake alilia nakusema “mama nisamehe, najuwa nilikosea na msamaha wako sitaupata kwasababu uko mavumbini”

Aliendelea kulia huku akiwa anaongea “lakini kwanini ulitoa laana ukijuwa siku zako ni chache na watu wasiyokuwa na hatia leo nimewaua leo wawili mmoja wapo akiwa rafiki wa boyfriend wangu’’ aliendelea kulalamika kwenye kaburi la mama yake Enjolata huku akiwa Analia.

Enjolata alikuwa Analia kwasababu alijuwa ipo siku hata boyfriend

wake atamua mwenyewe.  “Mama kama unanisikia naomba nisamehe” alisema Enjolata.

Alirudi nyumbani ikiwa nimuda wa saa moja usiku alipofika nyumbani akanyata ili lisijekutokea jambo jingine mamdogo wake naye asije kuiaga dunia.

Alipokwisha ingia jikoni akamkuta huku machozi yakiendelea kumtoka. Akiwa chumbani aliendelea kuwaza “ninamkosi lakini Derrick naye nimbishi’’  akiwa anawaza hivyo mala ujumbe ukaingia kwenye simu yake.

“Kesho tuonane” Enjolata naye akamjibu.

“sihitaji kuonana nawewe kwani siku ile ulikuwa na hasira zimeisha ila kwangu ndiyo zimeanza” mala tu baada ya kujibu hivyo ikambidi apige simu.

Enjolata hakupokea simu iliita karibia mala 10 hatimaye akaizima aliona kama usumbufu.

Siku hiyo ikawa imepita siku iliyofuata boyfriend wake akaja nyumbani kwao Enjolata.

“Hodi nimemkuta enjolata au?” alibisha hodi mala baada yakuingia eneo la nyumbani kwao Enjolata. Mama yake mdogo Enjolata akajibu “yupo lakini amefunga mlango hajafungua toka jana”

“kwanini anaumwa?” aliuliza boyfriend wake.

“hapana nikawaida yake kuna wakati anafanya hivyo nilisha mzoea”

“swa utamwambia nilikuja” alisema boyfriend wake nakuondoka.

*

Ilikuwa ni siku ya tatu Enjolata ikabidi atoke nje siku hiyo machozi hayakumtoka kwasababu alikuwa ameshatimiza kazi yake. Gafla akasikia kelele za vilio maeneo jirani yule kaka alipoteza maisha kwakupaliwa na chai akawa amekufa kwa namna hiyo.

Mala ujumbe kutoka kwa boyfriend wake ikaingia “Tafadhari sahau yote rafiki yangu amekufa nakuja kukupitia twende” ulikuwa ujumbe wa boyfriend wake.

Msibani mama mmoja alikuwa akilia nakusema “wewe unaye uwa watu bila hatiya kwanini unafanya hivyo” Enjolata anakosa amani moyo wake unapata maumivu makali na huku akimlaumu mama yake mzazi.

chanzo cha kifo chake marehemu kikaanza kusomwa mbele ya watu, “kijana huyu alimuaga mama yake akienda kulala nakumwambia mama mimi naenda kulala pumzi imekata nahisi sita amka tena nimefika mwisho”

Baada ya kukamilika kwa maziko Enjolata akarudi nyumbani kwao. Alitamani bora afe maana duniani yeye hana faida yoyote bali ana hasara kwa watu wengine.

siku iliyofuata rafiki yake Enjolata alikuja kumtembelea.

“Enjolata pole ya msiba”

“haina haja sina raha tena ya maisha” alisema Enjolata.

Wiki tatu baada ya msiba

Enjolata alikuwa akifua  mala anashituka nakumuona boyfriend wake. Enjolata akajiuliza akilini.

"Amefuata nini asubuhi hii yote!"

"Naona unahasira leo hasiara zako zitaisha nimechoka tena nimekuja kwaajili yako" alisema boyfriend wake.

"Nimechoka kuwa mpweke nataishi na nani na rafiki yanu amesha poteza maisha" alipomaliza kuzungumza maneno hayo boyfriend wake akawa akimsaidia kufua nguo.

"Sidhani kama hasira nilizonazo kama utaweza kuzitoa mpaka niamuwe mimi mwenyewe" alisema Enjolata.

"Yule dada uliyemuona kwenye mtandao mtafute ili uwe naye kwenye mahusiano" aliendelea kuongea Enjolata. Enjolata amuonyeshe wazi kuwa hakuwahi kumchukia mtu kiasi kile,

"ulichezea nafasi ulidhani mimi sipendi kujipodoa nakupendeza?" alipomaliza kuongea hivyo akaingiza neno.

"Ondoka mimitena basi moyo wangu nimeshaufunga na funguo na kufuli kuna mtu yupo wakuja kufunguwa"

"Enjolata unaongea nini!" alisema boyfriend wake huku akiendelea kuzungumza.

"Chuki yako imezidi asilimia 100 nashindwa kukuelewa lakini"

"kwa jinsi ninavyokupenda kukosea kupo tu naomba nisamehe" alisema boyfriend wake huku akiendelea kuongea.

"Sikujua kama chuki uliyonayo ni hatari hebu nionee huruma" aliongea kwa unyonge.

"Nimaumivu gani unayoniwekea Enjolata"  boyfriend wake anakuwa na ile hali ya kujishusha.

“kweli najuwa unanipenda lakini kwenye moyo wangu haupo” alipomaliza Enjolata akazibwa mdomo anapogeuka kuangalia aliyemziba mdomo anakuta ni rafiki yake na boyfriend wake.

“kwanini unafanya hivyo kwanini hutaki kusemehe” kisha anaendelea kutoa maneno.

“uliyeniuwa nilisha semehe kwasababu uliamua kunitoa duniani, na ndio maana roho yangu inahangaika kila kona ya duniani kwasababu siku ya kifo changu haijatimia kwa hiyo usinishangae”

Moyo wa Enjolata ukawa ukimwenda mbiao. Akikumbuka vizuri niyule aliyekuwa rafiki yake na boyfriend wake lakini yeye ndiyo alimuua.

“Amenisamehe mama yangu kwanini hataki kunisamehe toka amekufa”

Boyfriend wake alitaka wasiachane Enjolata akafikiria kisha akamwambia “kumbe kweli unanipenda mungu alinde penzi letu” boyfriend wake anamkumbatia huku akimwambia maneno mazuri.

“ Wewe ndiye wapekee mlinzi wa moyo wangu”

“Usijali lakini hujaona mtu amekufa mmh!”

“sijamuona kwani kipindi ulipokuwa tukiongea kunamtu alikuwa anatusikiliza?”

“kama nilihisi hivyo ila tuachane nayo” alisema Enjolata. “Ila nina girlfriend ambae ni noma unaweza hata kuniua kwa presha” alisema boyfriend wake.

“kumbe nawewe umeona ni vizuri tena shukuru mimi nibahati katika maisha yetu lakini kwenye moyo wangu nina kidonda tena kibichi”

“kuhusu nini?”

“maisha yangu sijui yatakuwaje”

“usijali nipo na nitaendelea kuwa nawe lakini yule mdada wa kwenye mtandao hakikisha unamtazama kila siku ambae nae anaitwa enjolata”

“Hapana sio mpenzi wangu usifikilie hivyo”

“hata mimi nafahamu nimependa iwe hivyo kwasababu anaendana namimi pia jina kama langu”

“lakini rafiki aliyefariki siku ile aliona uso wako ukiwa umejipodoa namimi kesho natamani nikuone kwasababu tangu tumeanza mauhusiano sijawaji kukuona” alisema boyfriend wake.

“Ndiyo maana  nimekwambia itazame picha hiyo”

“kwanini au kuna nini?”

“Hiyo picha nimimi girlfriend wako enjolata” boyfriend wake anashituka!. “kwanini ulinificha toka ile siku nimekuonyesha?” anapomaliza kuuliza hivyo kisha anaendelea kuzungumza.

“Ila asante kweli nimejuwa wewe ni mzuri tena kama malaika na ndiyo maana nahitaji nikuone uso wako kesho”

“mmmh haitakuwa rahisi siku nikiitaji utaniona siku hiyo itakuwa ya ndoa”

“ndoa?”

“ndio kwasababu itakuwa ndio mwisho wa maisha yako, nakwanini iwe hivyo” alisema Enjolata akiwa amegoma boyfriend wake asiweze kuona uso wake.

**

# SEHEMU YA 2

USIKU (NIGHT)

Enjolata akiwa chumbani kwake usiku anashtuka usiku wa manane. Akasikia sauti ile ambayo mama yake alimwambia siku ile alipomtamkia ile laana.

"Mwanangu mtu yoyote atakayeona sura ya uzui wako ukiwa umejipodoa atakufa isipokuwa kaka yako tu'' akawa anasikiliza mambo ambayo aliambiwa na mama yake siku ile yakupewa laana hiyo ambayo iligarimu maisha yake kwa namnafulani na kwa watu wengine.

Hiyo yote ilikuwa nikwasababu Enjolata alikataa kuolewa na kijina fulani ndipo mama yake alianza kutoa laana hiyo ambayo alimwambia. "UZURI WAKO UTAKUWA KIFO KWA WENGINE" iliweza kumalizika sauti hiyo ambayo ilikuwa niya mama yake.

Enjolata alijikuta akipata maumivu ya moyo huku akijisemea. "Bora nife kuliko kukaa hapa duniani kuliko kusababisha vifo vya watu" baada ya kuwaza hivyo Enjolata anachukua kisu nakutoka

ndani.

Alipotoka ndani alienda moja kwa moja mpaka makaburini ambako lilikuwepo Kaburi la mama yake alipokuwa amezikwa,

“Mama nimekuja kufa kwenye kaburi lako umeshindwa kunisamehe kosa nililofanya sasa niwakati wakukufuata huko mavumbini kusubiri hukumu” mala alipomaliza kuzungumza maneno hayo akajichoma kisu kabla haja kizamisha kisu kwenye mwili wake anakumbuka hajamuaga boyfriend wake Derrick.

Asubuhi

Enjolata alipokuwa akitaka kuamka anasikia maumivu kwenye eneo la tumbo lake. “Haya maumivu niya nini lakini mbona makali alafu kwenye tumbo langu” alipokuwa akishangaa huku akijishika eneo la tumbo lake anahisi ni kidonda.

Akiwa bado anapapasa nakutoa mkono wake anaona damu kisha anaanza kujiuliza “au niko kwenye siku zangu! lakini nilishatoka kwenye siku zangu’’ alipogeuza macho yake kuangalia pembeni anaona kisu kikiwa na damu.

Enjolata kumbukumbu zikamjia kuwa alitaka kujiuwa “hivi kilicho sababisha nijaribu kujiuwa ni nini lakini?” alijiuliza nakushindwa kupata jibu mala baada ya hapo ikabidi amjuze mama yake mdogo ili ampeleke hospital.

“mbona jana ulikuwa mzima hili jeraha umetoa wapi?”

“mimi sijui”

“na hichi kisu enjolata?” aliuliza mama yake mdogo kisha aliendelea kumuuliza tena.

“ulitaka kujiuwa”

“hapana ni ndoto ambayo nilikuwa nikiota hata mimi nashangaa!”

alisema Enjolata.

Hospital

Enjolata walipofika na mama yake mdogo hospital dokta akaliangalia lile jeraha kisha akasema. "jeraha lake sikubwa sana halijadhuru viungo vya ndani kwahiyo inabidi afungwe bandeji na apewe dawa za kukausha kidonda" zoezi lilifanyika lakurudi nyumbani.

"mamdogo ngoja nilale"

"sawa namimi ngoja niende kazini" mala gafla boyfriend wake akafika. "woooh! Mamdogo una masihara!"

"shikamoo nimemkuta enjolata?"

"ndiyo lakini muda mchache uliyopita tumetoka hospital"

"hospital! ulikuwa unaumwa?"

"hapana ni enjolata mi naelekea kazini"

"sawa" basi boyfriend wake Enjolata akaingia ndani na kumkuta Enjolata. Akamkuta Enjolata akiwa amelala akamuamsha.

"Enjolata…. enjolata?" Enjolata akaitika.

"Abee" kisha boyfriend wake akamuuliza tena .

''unaumwa nini?"

"yani unabahati ungenikuta nimekufa"

“kwanini?”  mala anapo uliza hivyo Enjolata akamuonyesha jeraha kwenye tumbo. “haaaa mungu wangu! nani aliye fanya hivi na anashida gani nawewe”

“siyo mtu mwingine nimimi mwenyewe”

“kwanini ulidondoka au?”

“hapana nilijichoma kisu minakupenda sana ila naomba tu utafute mwingine nahitaji kuondoka kwenda mbali ambako hutoniona maisha yako yote”

“siwezi maana mtu uliye moyoni mwangu niwewe tutaondoka wote”

“sio safari hizo unazosafiri kwa gari mpenzi wangu’’  boyfriend wake akarudi nyuma.

“una maanisha nini?”

“namaanisha nahitaji kufa sihitaji kuishi duniani”

“kama unamaanisha hivyo nikotayari nikamuone rafiki yangu”

“nataka nikwambie siri yangu kwasababu safari hiyo tutakuwa wote au utabaki duniani”

“Nikibaki nitakuwa mpweke duniani nakuwa kama kichaa sisi tuko pamoja wewe hata kama ugekuwa jini mimi nitakupenda” alisema maneno hayo boyfriend wake huku akiendelea kuongeza mengine.

“hata kama leo unataka kufa niko tayari kufa kwaajili yako”

Enjolata akavuta pumzi kisha akamuuliza “rafiki yako alifua?” kisha boyfriend wake akamjibu “ndio enjolata”

“je unajuwa kifo chake kilitokana na nini?”

“sikujuwa ilitokana nanini maana risala ya marehemu sikuelewa kabisa”

“Mimi enjolata ndie niliye muuwa kwasababu…..”

“hebu subiri kwanza unasema wewe ndie uliye muuwa rafiki yangu!” boyfriend wake alimpa nafasi Enjolata aendelee kuzungumza. Enjolata akawa akitokwa na machozi huku akimjibu.

“kwa sababu aliona uzuri wangu nikiwa nimejipodoa ndio maana huwa sitaki kujipodoa mbele yako kwa maana nawewe ungekufa” boyfriend wake anakuwa makini kumsikiliza huku akiwa kimya kwa muda.

“unakumbuka ile siku baada ya sherehe ya dada yako tutakosana na mtandio wangu ukachukua?”

“ndio nakumbuka” alijibu kwa utulivu.

“hiyo siku ndio aliyoniona rafiki yako”

“sasa siri yangu ndiyo hiyo utakapo niona nimejipodoa utakuwa nasiku tatu za kuishi” aliendelea kueleza “uzuri wangu anayetakiwa kuona nikaka yang utu wengine wote atakeona atakufa nilaana ya mama”

**

Kesho yake

Ilikuwa ni siku ambayo Enjolata alienda kuchapisha kadi za harusi. Kwasababu Enjolata aliona heri atimize ile ndoto yake yakuolewa na boyfriend wake Derrick itimie "ila najuwa kabisa nitakuwa naye siku tatu baada ya ndoa" aliwaza Enjolata.

Enjolata alikuwa akiwaza hivyo kwasababu alijuwa tu Derrick ataenda kufa nayeye ataenda kujiuwa na wote wataishia kaburini japokuwa watazikwa makaburi tofauti.

Akiwa anawaza akajiuliza tena "lakini kwanini Derrick afe kwasababu yangu?" aliendelea kuwaza juu ya hilo suala. "Derrick hapana abaki duniani hana haja yakufa" mala baada ya kuwaza hivyo yule dada aliyekuwa akiandaa kadi akawa amemaliza kuandaa kadi.

"Dada tayari kadi hizi hapa" Enjolata akashituka kutoka kwenye wimbi kubwa la mawazo alilokuwa nalo. "Samahani" alisema Enjolata kisha anachukua zile kadi nakuondoka huku akishika simu nakumpigia Derrick.

"halloo"

"ndio enjolata"

"nahitaji tuonane kwenye hotel ya jiburudishe" alisema Enjolata na boyfriend wake akamkubalia kuhusu kukutana hapo.

BAADA YA KUFIKA

"vipi safari nileo nini?"

"hapana wiki inayokuja siku ya jumapili" alisema Enjolata.

“unajuwa niya nini derrick?”

“ndio najuwa yakwenda kanisani”

“haaa haaaaa” alicheka Enjolata kisha akamwambia. “Niya harusi yetu kadi hizi hapa” aliongea huku akiwa anamuonyesha. “Eeh!” alishangaa Derrick.

Wakati Derrick akiwa anashangaa Enjolata akamwambia “lakini tutaishi siku tatu tu nabadaye tutaaga dunia” Derrick akawa akishangaa akiwa anashangaa Enjolata akamwambia.

“lakini usiruhusu kufa acha nife mimi peke yangu”

“enjolata unatamani niishi lakini nitaishi na nani?” alizungumza kwa hisia Derrick.

“Niache nisafiri nawewe nakupenda”

“sawa derrick nashukuru”

SIKU YA HARUSI

Wakiwa saloon kwaajili ya kufanyia make up Enjolata akamuuliza Derrick.

“nijipodoe au?”

“lazima ujipodoe maana safari inakaribia”

**

Ukumbi haukuwa na watu wengi kwasababu Enjolata alihofia kuweza kuuwa watu wengi. Hakutaka mamdogo wake kuhudhuria harusi hiyo na akaamuwa ifanyike nje na eneo la walipokuwa wanaishi.

Wakati Derrick anamfunua Enjolata moyo wake ulianza kumuuma akahisi kama moyo wake unakatwa vipande machozi palepale yakaanza kumtoka Enjolata akaanza kuwaza moyoni.

"Derrick anisamehe machozi haya yanahashiria kifo chake" watu wakapiga vigelegele nawengine wakishangaa bibiharusi akitokwa na machozi!.

Ndoa ikamalizika na Derrick akafanikiwa kumuoa Enjolata "kweli wewe ndiye yule wa kwenye mtandao sikufuta picha ile" alisema Derrick huku akiendelea kuzungumza na kustajabu uzuri wa Enjolata.

"uzuri wako ndiyo huu na uwona mbele yangu leo baada ya kukuoa!" lakini machozi hayakuacha kumtoka Enjolata yaliendelea kumtoka  kuna kiboksi Enjolata anakitoa kwenye begi lake.

"Derrick fungua hicho kiboksi"

"hicho ni kisu ambacho siku ya tatu utanichoma"

"Nitakuchoma wapi?"

"chini ya kitovu maana mimi ndiye nitakaye kuuwa kwa uzuri wangu"

"nitawezaje kumchoma mke wangu?"

“Derrick utaweza unaona haya machozi hayakomi, kwasababu yana hashiria kifo chako siku ya tatu utakufa nayo yatakoma kutoka” alisema Enjolata.

SIKU YA PILI

Enjolata akaondoka na Derrick mpaka kwa mama yake mdogo alipokuwa anafanya kazi. Enjolata alipofika akaweka bahasha sehemu alipokuwa amekaa mama yake mdogo.

Bahasha iliyokuwa imeandikwa “Usinitafute kwasababu nimekufa kwa laana yamama yangu nimimi enjolata” Enjolata mala baada ya hilo aliondoka nakurudi alipokuwa amekwishaanza kukaa na Derrick huku akimpatia Derrick kisu nakuondoka kwenda porini.

SIKU YA TATU

“Enjolata ninahisi macho mazito naona kiza mbele yangu nahisi mapigo ya moyo yanaacha kudunda mwili unapatwa na ubaridi nisaidie” alisema Derrick.

“Derrick tafadhari chukua kisu haraka unichome” dalili ambazo alizokuwa akikabiliwa nazo Derrick ilikuwa ni kifo kinakaribia.

Derrick alichukua kisu nakumchoma wote wakaanza kuitafuta pumzi wakipata pata bila mafanikio na ndipo moyo uliacha

kudunda na macho kufumba.

Enjolata na Derrick wakasafiri kutoka duniani nakuelekea kuzimu na safari yao iliishia walipo wekwa kaburini na kufukiwa na mavumbi.

"uzuri wangu umesababisha kifo changu na mpenzi wangu!!" yalikuwa maneno ya Enjolata alipokuwa akikata roho.

***

## SEHEMU YA 3

### SABABU YA KUPEWA LAANA

Enjolata alipofikisha umli wa miaka ya kuvunja ungo uzuri wake ulianza kuonekana. Nakumfanya kuonekana akiwa msichana mwenye mvuto kitu ambacho kilimfanya mama yake kujivunia kumzaa Enjolata au kumeta Enjolata duniani.

Enjolata alipohitimu elimu yake ya msingi yaani (darasa la saba) mambo yalizidi kuwa mengi kuhusiana na uzuri wake kwani hakuna mwanaume ambaye aliacha kumtolea macho.

Akiwa anasubiria matokeo ya kujiunga na kidato cha kwanza shangazi yake alikuja nyumbani kwao Enjolata nakumuomba mama yake aweze kwenda na Enjolata nyumbani kwake ili akasomee huko lakini mama yake Enjolata hakuwa tayari kwa hilo.

“Huko ni mjini haiwezekani akasomee huko kwasababu wahuni niwengi huko mjini” alisema mama yake Enjolata huku akiendelea kuzungumza “huku hapaki hata mafuta mwanangu lakini anavutia watu je huko mjini itakuwaje?”

“huko ataenda kuishi shuleni huku shule iko mbali hebu fikiria umbali anaotumia kwenda shuleni” alisema shangazi yake huku akiendelea kusema.

“ Umbali huo anaotumia ndiyo hatari zaidi ni bora akae shuleni atakuwa akirudi rikizo” alimuelewesha shangazi yake kwa maneno yale mama yake Enjolata akaruhusu Enjolata aweze kuondoka na shangazi yake kwenda mjini.

Mjini kwa shangazi yake

Nyumba ya sangazi yake ilikuwa nzuri na ilimshangaza Enjolata. Na matokeo yalipo kwisha toka Enjolata akawa amefauru, shangazi yake katika hali ya upendo akamfanyia sherehe ya yeye kufauru shangazi yake akaalika watu wengi.

Muda ulikwenda na watu wengine alianza kuondoka pale ilipofika saa tano usiku na muziki uliendelea na wengine wakabaki ili kukesha na muziki.

Kesho yake

Ilikuwa ni asubuhi shangazi yake alimpeleka mjini kwaajili ya kumnunulia vifaa vya shule. Enjolata akawa akishangaa mjini jinsi palivyokuwa pazuri na ilipofika siku ya kufungua shule aliwahi Enjolata na shangazi yake shuleni.

Kila aliyemuona Enjolata macho yalimtoka na ilikuwa kwa wote wasichana kwa wavulana. “Huu uzuri wa huyu dada sijawahi kuona!” yalikuwa majadiliano ya wanafunzi katika shule hiyo.

(Baadaye kidogo bwenini)

“habari ya wewe dada?”

“Nzuri”

“unaitwa nani?”

“Naitwa enjolata”

“Eeh jina lako linaendana na uzuri wako” alisema kijana huyo kisha akajitambulisha jina lake.

“Mimi naitwa emmanuel”

DARASANI

“jamani kidato cha kwanza jitahidini kuzungumza kingereza” alisema mwalimu aliyekuwa akisimamia kampeni ya kuzungumza kingereza shuleni.

“utakapo zungumza Kiswahili utapata adhabu'' alisisitiza mwalimu huyo.

Masomo yaliendelea na muda wakupata chai ya asubihi ulifika.

Katika purukushani zakutaka kwenda kuchukua kikombe Enjolata anampalamia kaka mmoja mwanafunzi mwenzake alafu Note book yake aliyokuwa ameshikilia.

Yule kaka ikaanguka chini Enjolata akaogopa kisha yule kaka akamwambia. “Hivi nyie kidato cha kwanza mnashangaa nini mpaka umeniangushia note book yangu naomba haraka” Enjolata akainama na kuchukua ile Note book alipoangalia kwenye bega anaona ni mwanafunzi wa kidato cha tatu.

Yule kaka aliporuhusu macho yake kumtazama Enjolata tu hakuruhusu macho yake yaweze kutazama mahali pengine isipokuwa kwenye uso wake Enjolata.

Mala akaja rafiki yake Enjolata aitwayee Emmanuela. “Mbona

umesimama hapa mpaka uji umeisha! Ila usijli nitakupunguzia”

“sawa emmanuela” alisema Enjolata wakaondoka kabla hawajafika mbali yule kaka akamuita Enjolata nakumpa Note book yake.

Wakiwa wanajisomea Enjolata hakuwa anajisikia vizuri hivyo ikabidi ampe rafiki yake Note book ampatie yule kaka aliyempa Note book, Enjolata hakuweza kubaki bwenini punde yule kijana akwa amefika nakumuulizia.

“vipi rafiki yako yuko wapi?”

“Anaumwa lakini kanipa note book yako nikupe”

“hapana mrudishie yeye ndiye anipatie wala siyo mwingine”

“haya nitamwambia” alisema rafiki yake Enjolata.

USIKU

“Enjolata yule kaka amekataa kuchukua note book yake kasema wewe mwenyewe ndiyo umpatie”

“Jamani! Ila nitajikaza nitampeleka  emmanuela twende nje maana sina usingizi”

“matroni akikuona hawezi kukuruhusu”

“tunamwambia tunaenda kujisomea”

“mimi nina usingizi wewe nenda”

“sawa ila narudi sasa hivi” alisema Enjolata.

Anapotoka Enjolata anakutana na matroni kisha anamuuliza.

“unaenda wapi?”

“naenda kujisomea”

“lakini mbona muda wakujisomea umeisha kwani we ni kidato cha kwanza?” alisema matroni.

“unatakiwa ukalale maana nyie mnasumbua” aliendelea kuongea matroni. Mara baada yakumaliza matroni aliondoka Enjolata akabakia mwenyewe huku akijiuliza.

“Niende kulala au nikajisomee?” alipokuwa akijiuliza hivyo akili ikamjia heri aende kujisome. Alipofika alikuta kila mtu akiwa na tochi ila yeye tu ndiyo hakuwa na tochi.

“Nitajisomeaje?” alijiuliza mwenyewe wakati akiwa anajiuliza hivyo alikuwa amesimama kisha mtu mmoja akamuuliza.

“wewe nani mbona unakuja unasimama nakuondoka?” aliuliza mtu huyo kisha akaendelea kuzungumza.

“nyie ndio mnao chukua akili zetu kwanza wewe ni kidato cha ngapi?” akiwa anamuongelesha nikama akawa amekwishaanza kuvutiwa na uzuri wa Enjolata.

“wewe kisogo hebu toka hapa nakelele zako” alisema kiongozi wa darasa.

“sawa monitor”

“wewe mdada hebu njoo uniambie unatafuta nini?” Enjolata mala baada ya kuambiwa hivyo akamfuata pale alipokuwa amekaa ile anamfuata tu umeme ukarudi yule jamaa akamtzama.

“Enjolata niwewe!”

“ndio lakini note book yako sijaja nayo”

“usijali hebu kaa”

(Baada ya kukaa)

“usiniogope sawa”

“Lakini ndio umekuja huku ulikuwa unanitafuta mimi sindio”

“hana nilikosa usingizi nikaona bora nije kujisomea”

“laikini ulijichanganya kwenda sehemu ya kujisomea huku wanakaa kidato cha tatu’’ aliendelea kuzungumza huku kimpa maneno yakuonyesha kumjali.

“ukiwa nashida yoyote kwenye masomo nitafute nitakusaidia’’ aliongea nabado maneno hayakumuisha.

” lakini wewe mzuri sana kama malaika napenda kukuangalia uso kwa uso’’ aliongea nakuonyesha hisia za kweli kuhusu uzuri wa Enjolata.

Akawa akimtazama kwa ukaribu zaidi kisha akasema.

“wewe ni mzuri kaa ukijuwa hilo” Enjolata mala baada ya kuwa amepata ndoto hiyo akapiga kelele Emmanuela akamuuliza.

“nini mbona kelele!”

“Nimeota ndoto mbaya” alisema Enjolata.

Enjolata alipelekwa mahali ambapo kidato cha kwanza walikuwa wakikaa. Alipofika anakuta muda ukiwa umekwisha wakusoma ndipo aliyekuwa akimuongoza akamwambia.

“kumbuka jina langu naitwa gervas basi nenda ukalale enjolata” Enjolata alitoka akiwa amejawa na uoga moyo nao ukiwa unamdunda.

Enjolata alihisi ni ndoto lakini ndiyo ulikuwa uhalisia wa kweli. Yule kaka alionyesha kumpenda Enjolata lakini binti Enjolata hakujuwa ikiwa nikatika namna ya mapenzi.

ASUBUHI

Matroni tayari alikuwa amesha wasili kwaajili ya kuamsha wanafunzi kuoga pamoja na mengineyo.

“lakini emmanuela yule mkaka namuogopa”

“kwanini mbona hanashida”

“jana kanikumbatia anasema mimi mzuri” alisema Enjolata huku akionyesha kuchukizwa.

“hata kama mimi sijapenda”

“sasa wewe kwani sio mzuri enjolata?” aliuliza nakugundua atakuwa amechukia Enjolata kisha akamwambia.

“Basi uje umwambie asikuzoee’’ wanamaliza kuzungumza nakuelekea darasani kwaajili ya kwenda kuanza masomo.

“kidato cha kwanza jamani” ilikuwa sauti ya mwalimu ikisikika.

“Ndiyo mwalimu” waliitikia wanafunzi “ninatangazo kuhusu siku ya juma pili itakuwa siku ya kutembelewa na wazazi”

“ndiyo mwalimu” waliitikia wanafunzi kwasababu kila mmoja aliingiwa na furaha.

“basi badaye mtakuja ofisini kwaajili ya kuwajulisha”

## Kuondoka kwenda Breack fast

“Emmanuela nisaidie kitu’’ (alisema Enjolata)

“kitu gani?”

“Note book ya yule mkaka”

“nimpelekee?”

“ndio”

“mwambie mwalimu ameniita ofisini kwake sawa’’ Emmanuela akaichukua ilikumpelekea Gervas.

“mambo?”

“poa”

Vipi mbona uko mwenyewe!”

“Enjolata ameitwa na mwalimu ofisini”

“kumbe”

“ndiyo lakini ameniambia nikupatie not book”

“ooh hamna shida” alisema kaka huyo kisha anamueleza tena “mwambie nahitaji kuzungumza naye”

“sawa nitamwambia”

Siku zikawa zimeenda na masomo yakaendelea kama kawaida. Sikuu hii Enjolata alikuwa amekaa na rafiki yake Gervas akaja nakumsalimia “mambo?”

“poa”

“samahani emmanuela unaweza kutupisha”

“Kwanini rafiki yangu akupishe kwani yeye sio mtu?”

“hapana nahitaji kuzungumza na wewe”

“kwani huwezi kuzungumza emmanuela akiwepo?”

“sitaki alafu usiwe unanitafuta kaa na darasa lako sio sisi kidao cha kwanza” alisema Enjolata. “Enjolata unajuwa mimi nachotaka kukuambia lakini?”

“sihitaji kujuwa”

“kwani nimekosea nini?”

“unatabia mbaya na tayari nimekwisha ripoti kwa mwalimu”

“tabia gani?”

“usi niulize maswali”

“sawa badae” (kisha Gervas akaondoka)

“emmanuela nimemkomesha”

“hapo ataacha kukuzoea”

“ila rikizo pia zimebakia wiki mbili”

KESHO YAKE

Gfla Enjolata aliitwa Ofisini ikiwa ni majira ya saa 3:30 asubuhi akwa amekuja shangazi yake na Enjolata. Baada ya mazungumzo shangazi yake alimwambia.

“Nimekuja kukuombea ruhusa enjolata kwahiyo unatakiwa kuchukua vitu vyako nakuondoka” Enjolata alienda kuchukua vitu vyake nakumuaga rafiki yake.

Baada yakufika kwa shangazi yake shangazi alianza kumuelezea sababu ya kumuombea ruhusa. “Mama yako anaumwa inabidi urudi kijijini kwanza” alisema shangazi yake akiwa anamuweka sawa.

“Unatakiwa kwenda kumuuguza” Enjolata siku iliyofuata alienda kijijini na alipofika akapokelewa na mmoja ya majirani yao.

Anapoingia ndani anamkuta mama yake akiwa anaumwa lakini ilikuwa kawaida na alikuwa amelala kitandani.

"shika moo mama"

"malahaba za huko ulikotoka'?"

"ni nzuri lakini pole na ugonjwa"

"yaani mwili hautaki niiname na karibia kazi zote zinahitaji kuinama" alisema mama yake "Nimeona uje unisaidie mkifungua shule nami utakuka nimekwisha pona" aliendelea kusema mama yake mdogo.

"Mungu atakusaidia mama"

"usijali mungu atafanya kuna viazi hapo kula" mama yake aliendelea kuzungumza kwa furaha.

"Marafiki zako walikuwa wanakuulizia nikawambia umeenda mjini" akamwambia tena.

"ila wengi wao wameishia njiani kwenye masomo na wengine wameolewa"

"kumbe!" alisema Enjolata hukua akiweka ukimya kumsikiliza.

"Hata wewe ungakuwa hapa kijijini ungekuwa umeshaolewa ila soma ufike mpaka chuo kikuu"

"sawa mamdogo wewe lala ngoja mimi nikakusanye kuni kule porini"

"sawa kuwa makini na uzuri wako"

"sawa mama"

"maana kila kijana wa huu mtaa anatamani uwe mke wake"

Basi Enjolata baada ya hayo yote aliendelea kumuuguza mama yake na siku zikaenda na ikabakia siku tatu iliaweze kurudi shuleni.

Rikizo nayo ikawa imekwisha hali ya mama yake ikawa imebadirika gafla ikawa tofauti na ile ya mwanzo alishindwa kula hata chakula kwasababu ya mdomo kuvimba pamoja na tumbo.